



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAMISEMI



HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA

Simu: Mkuu wa Shule 0754048835, M/Mkuu wa Shule 0757612107
Mwl. Malezi 0655678821
Email: iyungasecondary@gmail.com
Website: www.iyungatechnicalschool.sc.tz

SHULE YA SEKONDARI IYUNGA
S.L.P. 701
MBEYA.

Unapojibu tafadhali taja:

KUMB NA. IYU/U/12

08/12/2020

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

.....
S.L.P.

.....

Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI IYUNGA,
HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA, MKOA WA MBEYA
KIDATO CHA KWANZA 2021

1. Utangulizi:-

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020.

Shule ya Sekondari Iyunga ipo umbali wa kilometa tano (5) Magharibi mwa jiji la Mbeya. Usafiri wa basi dogo (Hiace) kutoka kituo kikuu cha mabasi Mbeya unapatikana na nauli ni shilingi mia nne tu (400/=)

Muhula wa masomo unanza tarehe 11/01/2021 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 10/01/2021

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2.1 Sare ya shule

- (a) Suruali mbili (2) rangi ya kaki inayofanana kama ya polisi, ya heshima siyo "modo" (iwe na marinda mawili).
- (b) Mashati mawili rangi nyeupe mikono mifupi yote yawe marefu yakuweza kuchomekewa kwenye suruali.
- (c) Tai nyeusi ndefu ya kufika kiunoni
- (d) Viatu vya shule vyeusi vya ngozi jozi 2. Viwe vya heshima vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba.
- (e) Soksi rangi nyeusi jozi mbili.
- (f) Sweta rangi ya bluu (Rangi ya kizibo cha biki) shingo ya "V"
- (g) Mkanda mweusi wa suruali usio na picha wala madoido.
- (h) Fulana (T-shirt) mbili rangi ya kijivu, moja itatumika kama shamba dress na nyingine kwa ajili ya michezo. Fulana iwe ya kola ya duara na siyo vinginevyo.

